# *KATIBA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR 1979*

Kimepigwa Chapa na Idara ya Upigaji Chapa,
Zanzibar.
1979

## KATIBA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR YA MWAKA 1979

### YALIYOMO

Ibara Kichwa cha Habari

UTANGULIZI

MISINGI YA KATIBA

SURA YA KWANZA
ZANZIBAR, CHAMA NA WATU

SEHEMU YA KWANZA

ZANZIBAR NA CHAMA

1. Zanzibar
2. Eneo la Zanzibar na mipaka ya Mikoa, Wilaya n.k.
3. Chama na Mamlaka yake.

SEHEMU YA PILI

4. Haki ya kupiga kura.

SURA YA PILI

KIONGOZI WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA UCHAGUZI WAKE

SEHEMU YA KWANZA

5. Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar na Madaraka yake.

SEHEMU YA PILI

6. Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar.
7. Muda wa kuendelea na madaraka ya Mwenyekiti.
8. Utekelezaji kazi na shughuli za Mwenyekiti wakati hayupo.
9. Mshahara na malipo mengineyo ya Mwenyekiti.
10. Mwenyekiti hatashitakiwa wala kudaiwa Mahakamani wakati akiwa kazini.
11. Tafsiri.

SURA YA TATU

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

SEHEMU YA KWANZA

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

12. Madaraka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## SURA YA NNE

### MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA YA ZANZIBAR, BARAZA LA JUU NA UTARATIBU WA KUPELEKA MAAGIZO YALIYOMO KATIKA HATI ZILIZOTOLEWA NA MAHAKAMA

### SEHEMU YA KWANZA

44. Mahakama Kuu ya Zanzibar.
45. Uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu.
46. Muda wa kushika madaraka wa Majaji.
47. Kiapo cha Majaji.
48. Mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

### SEHEMU YA PILI

### MADARAKA YA KUAJIRI MAHAKIMU NA WATUMISHI WENGINE WA MAHAKAMA ZA ZANZIBAR NA TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA

49. Tume ya Kuajiri ya Mahakama.
50. Madaraka ya kuajiri Mahakimu na Watumishi wengineo na Mahakama.

### SEHEMU YA TATU

### BARAZA LA JUU

51. Baraza la Juu.
52. Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza la Juu.
53. Kazi za Baraza la Juu.
54. Mahakama ya Rufaani ya Tanzania.
55. Utekelezaji wa maagizo ya Mahakama utafanywa nchini Tanzania kote.

## SURA YA TANO

### MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

56. Mahakama Maalum ya Jamhuri ya Muungano.

## SURA YA SITA

### TUME YA KUDUMU YA MIPANGO

57. Baraza la Mipango.
58. Wajumbe wa Baraza.
59. Muundo wa shughuli za Tume ya Kudumu ya Mipango.

## SURA YA SABA

### SEHEMU YA KWANZA

### TUME YA KUDUMU YA UCHUNGUZI

60. Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.

SEHEMU YA PILI

TUME YA TABIA YA VIONGOZI

61. Tume ya Tabia ya Viongozi.

SURA YA NANE

MASHARTI KUHUSU MAMBO YA FEDHA ZINAZOHUSIKA NA HAZINA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

62. Masharti ya kutoza kodi.
63. Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
64. Masharti ya kutoa fedha za matumizi kutoka Mfuko Mkuu.
65. Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.
66. Kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria kuanza
67. Mfuko wa Matumizi ya Dharura.
68. Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
69. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
70. Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

SURA YA TISA

MADARAKA MIKOANI—KAMATI ZA MAPINDUZI

71. Serikali za Mitaa.
72. Kazi za Kamati za Mapinduzi.
73. Tume ya Uchaguzi.

SURA YA KUMI

TUME YA UCHAGUZI YA SERIKALI YA ZANZIBAR

SURA YA KUMI NA MOJA

IDARA MAALUM KWA SHUGHULI ZA ZANZIBAR

JESHI LA KUJENGA UCHUMI, KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO NA CHUO CHA MAFUNZO

74. Idara Maalum za Serikali ya Zanzibar.

SURA YA KUMI NA MBILI

UFAFANUZI

75. Utaratibu wa kujiuzulu kwa mwenye madaraka yoyote chini ya Katiba hii.
76. Utaratibu wa kuteua mtu kushika madaraka kwa muda.
77. Utaratibu wa Sheria za Muungano kutumika Zanzibar.
78. Tume ya Uchunguzi.
79. Tafsiri ya Katiba.
80. Ufafanuzi.
81. Jina kamili la Katiba na tarehe ya kuanza kutumika Katiba.

# KATIBA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR YA MWAKA 1979

## UTANGULIZI

## AZIMIO LA BARAZA LA MAPINDUZI LA KUWEKA KATIBA YA SERIKALI YA ZANZIBAR

Kwa kuwa mkutano maalum wa Baraza la Mapinduzi wa tarehe 5 Februari, 1964, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ulielewa na kukubali kwamba jukumu letu katika historia ya Watu wa Zanzibar ni kuimarisha Umoja, kuendeleza Mapinduzi ya Kijamaa katika Zanzibar na kusukuma Mapambano ya ukombozi na harakati za Mapinduzi nchini, katika Afrika na duniani kote;

Kwa kuwa tunatambua kwamba Tanzania Visiwani ni jamii ya Watu walio chini ya Serikali moja ya Kidemokrasi yenye lengo maalum la kuweka Utawala wa Sheria;

Kwa kuwa tunatambua kwamba Umoja wa Wananchi wa Zanzibar unatokana na ushirikiano wa miaka mingi tangu wakati wa mapambano ya kupigania Uhuru hadi kufikia daraja hii ya mafanikio, na unatokana na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea;

Kwa kuwa tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na Viongozi wa Mapinduzi, wakiongozwa na Mwasisi wa Chama cha ASP na Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima, kizazi baada ya kizazi katika kupambana na Ukoloni, Ubepari, Kiburi, Unyonge, Uonevu na Dharau, na badala yake kudumisha Uhuru na Umoja, Haki na Usawa, Heshima na Utu;

Kwa kuwa tunatambua kwamba kuweko kwa Chama cha Mapinduzi kunaongeza upeo wa nguvu na Umoja wetu katika kuendeleza mapambano ya kujenga ujamaa nchini na kushiriki kwa pamoja na kikamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar, ya Tanzania, ya Afrika na ya Dunia;

Kwa kuwa tunatambua kwamba mafundisho na mawazo ya Kimapinduzi yatalindwa, yataendelezwa na kudumishwa kwa misingi ya Kidemokrasi; na

Kwa kuwa tunatambua kuwa mapambano ya kujenga Ujamaa katika Zanzibar na kushiriki kwetu kikamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar kunahitaji SHERIA madhubuti itakayowaongoza watu Ki-Katiba, kutokana na fikra za Wafanyakazi na Wakulima;

KWA HIVYO BASI:

BARAZA LA MAPINDUZI, katika kikao chake maalum cha tarehe 5 Oktoba, 1979, hadi tarehe 12 Oktoba, 1979, chini ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ndugu Aboud Jumbe, kwa kauli moja limepitisha Sheria ya Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1979, amabyo kwa kifupi itajulikana kama "KATIBA YA ZANZIBAR" kwa misingi ifuatayo:—

## MISINGI YA KATIBA

LENGO NA MADHUMUNI YA KATIBA HII NI UHURU NA UMOJA, HAKI NA USAWA, UDUGU NA AMANI, MAMBO AMBAYO MISINGI YAKE NI HII IFUATAYO:—

A. KWAMBA—

(i) binaadamu wote ni sawa;

(ii) kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake;

(iii) kila mtu anayo haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, hifadhi ya kuishi kama mtu huru na hifadhi ya mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa Sheria;

(iv) kila mtu anayo haki ya uhuru wa kuamini dini anayotaka, uhuru wa kutoa mawazo yake, uhuru wa kwenda anakotaka na uhuru wa kushirikiana na watu wengine, ili mradi havunji Sheria au taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria;

(v) kwa kutumia vikao vilivyowekwa, kila raia anayo haki ya kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi wa mambo ya Taifa na yanayomuhusu;

(vi) kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake.

B. KWAMBA Ujamaa na kujitegemea ndiyo njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio sawa na huru—

C. KWAMBA kila jamii inao wajibu wa—

(i) kuheshimu na kuthamini utu wa kila binadamu pamoja na haki zake nyingine;

(ii) kulinda na kutekeleza maagizo ya Sheria za nchi;

(iii) kutekeleza shughuli za Serikali kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine;

(iv) kuhakikisha kwamba katika nchi kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayompatia mtu riziki yake;

(v) kuweka na kudumisha heshima ya binadamu kwa kufuata barabara Kanuni za Tangazo la Dunia kuhusu haki za Binadamu;

(vi) kuhakikisha kwamba Serikali na vyombo vyote vya Umma vinatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu;

(vii) kuhakikisha kwamba katika nchi hakuna namna yoyote ya dhulma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu na upendeleo;

(viii) kuhakikisha kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi, hasa jitihada za kuondosha umasikini, ujinga na maradhi;

(ix) kuhakikisha kwamba Serikali inamiliki njia kuu za uchumi;

(x) kuhakikisha kwamba Serikali inatawala kwa misingi ya Kidemokrasi na ya Kijamaa.

D. KWAMBA ni wajibu wa kila mtu kuamini kwamba kazi ni kipimo cha utu, na kutekeleza imani hiyo kwa vitendo—

E. KWAMBA haki zote za binadamu zaweza tu kudumishwa na kulindwa barabara, na wajibu wa kila mtu waweza tu kutekelezwa kwa ukamilifu, katika jamii yenye demokrasi na yenye Serikali ambayo hutekeleza shughuli zake chini ya usimamizi wa Baraza la Wawakilishi linalowakilisha wananchi, na pia katika jamii yenye Mahakama ambazo hutekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote au kuingiliwa na yeyote.

## SURA YA KWANZA

### ZANZIBAR, CHAMA NA WATU:

### SEHEMU YA KWANZA

### ZANZIBAR NA CHAMA:

1. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar

2.—(1) Eneo la Zanzibar ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na bahari yake ambayo kabla ya Muungano ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Eneo la Zanzibar. na Mipaka ya Mikoa, Wilaya n.k.

(2) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu au kukubaliwa na Chama cha Mapinduzi.

3.—(1) Chama cha Mapinduzi (kwa kifupi "CCM") ndicho Chama cha siasa pekee katika Tanzania na ndicho chenye madaraka ya mwisho katika mambo yote kwa mujibu wa Katiba ya Chama. Chama na Mamlaka yake.

(2) Shughuli zote za vyombo vyote vya umma katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitaendeshwa chini ya uongozi na usimamizi wa Chama.

(3) Masharti yote yaliyomo katika Katiba hii yatatakiwa yatekelezwe kwa kuzingatia wakati wote madaraka ya Chama kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (1), ya (2) ya Ibara hii.

### SEMEHU YA PILI

### WATU

4.—(1) Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi. Haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti mengineyo ya Katiba hii na ya Sheria inayotumiwa nchini Tanzania au Zanzibar kuhusu mambo ya uchaguzi. Haki ya kupiga kura.

(2) Kutegemeana na aina ya uchaguzi unaohusika Zanzibar, masharti kuhusu mambo yafuatayo yanaweza kuwekwa na Sheria iliyotungwa na ama Bunge la Jamhuri ya Muungano au na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar:—

(a) utaratibu wa kuandikisha wapiga kura katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na wa Wabunge, au uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar na wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(b) kutaja sehemu na nyakati za kuandikisha wapiga kura na za kupiga kura;

(c) utaratibu wa kumwezesha mpiga kura aliyejiandikisha sehemu moja kupiga kura sehemu nyingine na kutaja masharti ya utekelezaji wa utaratibu huo;

(d) kutaja kazi na shughuli za Tume ya Uchaguzi inayohusika na utaratibu wa kila uchaguzi ambao utaendeshwa chini ya uongozi na usimamizi wa Tume ya Uchaguzi inayohusika.

## SURA YA PILI

### KIONGOZI WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA UCHAGUZI WAKE

### SEHEMU YA KWANZA

Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar na Madaraka yake

5.—(1) Kutakuwa na Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar ambaye ndiye atayekuwa Rais wa Zanzibar na Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vile vile Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atashika na kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii pamoja na vifungu vyote vinavyohusika vya Katiba ya Chama na ya Jamhuri ya Muungano ya 1977.

(3) Mbali na kuzingatia siasa na maagizo ya Chama, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote katika utendaji wa kazi na shughuli zake, isipokuwa kama Sheria inaagiza vyenginevyo.

(4) Pamoja na madaraka yake yote mengine, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ndiye atakayewateua na kuwakabidhi madaraka Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Mawaziri na Manaibu Waziri ambao watawasadia Mawaziri katika utekelezaji wa shughuli zao katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### SEHEMU YA PILI

### UCHAGUZI WA KIONGOZI WA SERIKALI YA ZANZIBAR

Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar.

6.—(1) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atachaguliwa na Wananchi kwa masharti ya Katiba hii na kwa mujibu wa Sheria itakayoweka masharti kuhusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa kufuata masharti ya Katiba hii.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama Kiongozi wa Serikali na Rais wa Zanzibar atachaguliwa kila mara litokeapo mojawapo ya mambo yafuatayo:—

(a) baada ya kujiuzulu Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar;

(b) baada ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kufariki;

(c) ikiwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(d) baada ya Baraza la Wawakilishi kuvunjwa au wakati wowote ule ambao uchaguzi wa viongozi wote utaitishwa kufanywa kwa mujibu wa Katiba ya Chama au Sheria inayohusika;

(e) baada ya kuthibitishwa kwa mujibu wa Sheria hii kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar hawezi kutekeleza kazi na shughuli zake na ikiwa hali hiyo ya kutomudu kazi itaendelea kwa muda zaidi ya miezi sita.

(3) Wakati wa kuchagua Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar ukiwadia kutokana na jambo lolote lililotajwa katika Ibara ndogo (2) ya Ibara hii ili Kamati Maalum ya Kamati Kuu ya Chama ilioundwa na Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Chama (kwa ajili ya kuangalia na kusimamia shughuli zote za Serikali kwa upande wa Tanzania Visiwani) itakutana na kupendekeza majina ya watu yasiopungua mawili kutoka Tanzania Visiwani waliotimiza umri usiopungua miaka thelathini wanaofaa kuwa ndio watu pekee watakaosimama katika uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar.

(4) Majina ya watu hao waliyopendekezwa katika uteuzi wa mwanzo uliofanywa na Kamati Maalum kwa mujibu wa masharti ya Ibara ndogo ya (3) yatawasilishwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama ambayo nayo itafanya mkutano kwa ajili ya kufanya uteuzi wa mwisho wa mtu atakaesimama katika Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii.

(5) Baada ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama kuthibitisha uteuzi wa mtu ambaye jina lake limewasilishwa kwake, mtu huyo atasimama katika uchaguzi na wananchi watapiga kura ya kumkubali au kumkataa na kutegemea matokeo ya kura hiyo mambo yatakuwa ifuatavyo:—

(a) ikiwa zaidi ya nusu ya wapigaji kura wote wamemkubali mgombea kiti, basi mtu huyo atakuwa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar na Tume ya Uchaguzi itamtangaza kuwa amechaguliwa;

(b) ikiwa zaidi ya nusu ya wapiga kura wote wamemkataa mgombea kiti, basi mtu huyo atakuwa hakuchaguliwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar na katika hali hiyo Kamati Maalum ya Kamati Kuu ya Chama (kwa ajili ya kuangalia na kusimamia shughuli zote za Serikali kwa upande wa Tanzania Visiwani) itakutana tena na kutoa pendekezo la majina ya watu wengine kutoka Tanzania Visiwani waliotimiza umri usiopungua miaka thelathini na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama halikadhalika itakutana tena na kufanya uteuzi wa mwisho kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (4) na hatimae Uchaguzi utafanywa, kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo.

(6) Iwapo mtu ametangazwa na Tume ya Uchaguzi kwamba amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya 5 (a) basi hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

Muda wa Kuendelea na madaraka ya Mwenyekiti.

7.—(1) Isipokuwa kama atajiuzulu au atafariki mapema zaidi, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ataendelea kufanya kazi yake mpaka mtu atakaechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar utakaofuata atakaposhika madaraka yake.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ataapishwa kiapo kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Utekelezaji kazi na shughuli za Mwenyekiti wakati hayupo.

8.—(1) Endapo Baraza la Mapinduzi litaona kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hawezi kumudu kazi zake kwa sababu ya maradhi, basi Baraza hilo laweza kuwasilisha kwa Jaji Mkuu azimio la kumwomba Jaji Mkuu athibitishe kwamba Mwenyekti hamudu kazi zake kwa sababu ya maradhi. Baada ya kupokea azimio kama hilo na baada ya kufikiria maalezo ya daktari, Jaji Mkuu atawasilisha kwa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama taarifa ya kuthibitisha kwamba Mwenyekiti hamudu kazi zake kwa sababu ya maradhi. Kila itakapotokea taarifa ya namna hiyo, Halmashauri Kuu ya Taifa itatoa tamko kwamba Mwenyekiti hamudu kazi zake kwa sababu ya maradhi, na iwapo Halmashauri Kuu ya Taifa haitabatilisha tamko hilo kutokana na Mwenyekiti kupata nafuu na kurejea kazini, basi itahesabiwa kwamba Mwenyekiti hayupo. Katika hali hiyo na pia ikitokea kuwa kiti cha Mwenyekiti kiwazi, au kwamba Mwenyekiti hayupo Zanzibar au nje ya Tanzania, basi wakati wote Mwenyekiti atakapokuwa hayupo kazi na shughuli za Mwenyekiti zitatekelezwa na mmojawapo wa watu wafuatao, kwa kufuata orodha kama ilivyopangwa, yaani—

(a) Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi aliyeteuliwa na Mwenyekiti kwa ajili hiyo, au kama naye hayupo, basi

(b) Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi aliyechaguliwa kwa ajili hiyo na Baraza la Mapinduzi.

(2) Endapo itatokea kuwa kiti cha Mwenyekiti kiwazi kutokana na Mwenyekiti kujiuzulu au kufariki, au kwamba Mwenyekiti hayupo Tanzania, au kuwa Mwenyekiti hamudu kazi zake kwa sababu ya maradhi, na Jaji Mkuu, baada ya kufikiria maelezo ya daktari, atawasilisha kwa Halmashauri Kuu ya Taifa taarifa ya kuthibitisha kwamba Mwenyekiti hamudu kazi zake, wakati ambao hayupo Waziri anayeweza kutekeleza kazi na shughuli za Mwenyekiti kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1), na

ikiwa hawapo Mawaziri wengine katika Baraza la Mapinduzi wanaoweza kukutana kwa shughuli yoyote, basi katika hali hiyo mambo yatakuwa ifuatavyo—

(a) taarifa ya uthibitisho itakayowasilishwa na Jaji Mkuu kwa Halmashauri Kuu ya Taifa itahesabiwa kuwa ni halali kama kwamba imetolewa naye baada ya kupokea azimio la Baraza la Mapinduzi la kumwomba atoe taarifa hiyo, na haitachunguzwa imetolewa bila ya Jaji Mkuu kupokea kwanza azimio la Baraza la Mapinduzi; na

(b) Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama itamchagua raia mmoja kutoka Tanzania Visiwani aliyetimiza umri wa miaka thelathini atakayeonekana anafaa, kutekeleza kazi na shughuli za Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar wakati wote Mwenyekiti atakapokuwa hayupo kazini au mpaka atakapopatikana Waziri atakayetekeleza kazi na shughuli hizo kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1).

(3) Iwapo itatokea kuwa—

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hayupo katika mji wa Makao Makuu ya Serikali; au

(b) Mwenyekiti hayupo Zanzibar au Tanzania kwa muda ambao Mwenyekiti anafikiria utakuwa si mrefu; au

(c) Mwenyekiti ni mgonjwa na anatumaini kuwa atapata nafuu baada ya muda si mrefu;

na Mwenyekiti akiona kuwa inafaa kuwakilisha kwa muda huo madaraka yake, basi aweza kutoa maagizo kwa maandishi ya kumteua Waziri kwa ajili ya kutekeleza kazi na shughuli za Mwenyekiti wakati Mwenyekiti hayupo. Waziri anayehusika, atatekeleza madaraka hayo ya Mwenyekiti kwa kufuata masharti yoyote yatakayowekwa na Mwenyekiti.

Isipokuwa kwamba masharti yaliyomo katika Ibara hii ndogo yafahamike kuwa hayapunguzi wala kuathiri uwezo wa Mwenyekiti alio nao kwa mujibu wa Sheria nyingine yoyote wa kuwakilisha madaraka yake kwa mtu mwingine yeyote.

(4) Mwenyekiti aweza, akiona inafaa kufanya hivyo, kumwagiza kwa maandishi Waziri yeyote kutekeleza kazi na shughuli zozote za Mwenyekiti ambazo Mwenyekiti atazitaja katika maagizo yake, na Waziri aliyeagizwa hivyo kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo, atakuwa na mamlaka ya kutekeleza kazi na shughuli hizo kwa kufuata masharti yoyote yaliyowekwa na Mwenyekiti, lakini bila ya kujali masharti ya Sheria nyingine yoyote; Isipokuwa kwamba—

(a) iwapo Mwenyekiti amemwagiza Waziri yeyote kutekeleza kazi na shughuli zozote za Mwenyekiti kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo, basi ifahamike kuwa maagizo hayo hayatamzuia Mwenyekiti kutekeleza kazi na shughuli hizo yeye mwenyewe.

(5) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa madhumuni ya ufafanuzi wa ibara ndogo ya (1) na ya (2)—

(a) kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1) na ya (2), Mwenyekiti hatahesabiwa kuwa hayupo Zanzibar au Tanzania kwa sababu tu ya kupitia nje ya Tanzania wakati yuko safarani kutoka sehemu moja ya Zanzibar au Tanzania kwenda sehemu nyingine, au kwa sababu kwamba ametoa maagizo kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) na maagizo hayo bado hayajabatilishwa;

(b) kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1) peke yake, mkutano wa Baraza la Mapinduzi uliofanywa kwa ajili ya kuwasilisha kwa Jaji Mkuu azimio kuhusu hali ya Mwenyekiti utahesabiwa kuwa ni mkutano halali hata kama mjumbe mmojawapo wa Baraza hilo ikiwa litaunga mkono kwa kauli ya wajumbe walio wengi waliohudhuria mkutano na kupiga kura.

(6) Bila ya kujali masharti yaliyoelezwa hapo awali katika ibara hii, mtu atakayetekeleza kazi na shughuli za Mwenyekiti kwa mujibu wa ibara hii hatakuwa na mamlaka ya kumwondoa mjumbe wa Baraza la Mapinduzi au Waziri katika madaraka yake.

(7) Waziri, Mjumbe Mwakilishi au mtu mwengine yoyote atakayetekeleza kazi na shughuli za Mwenyekiti kwa mujibu wa masharti ya ibara hii hatapoteza kitu chake katika Baraza la Wawakilishi wala hatapoteza sifa zake za kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti kwa sababu tu ya kutekeleza kazi na shughuli za Mwenyekiti kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

**Mshahara na malipo mengine ya Mwenyekiti.**

**9.**—(1) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atapokea mshahara na malipo mengineyo, na atakapostaafu atapokea malipo ya uzeeni, kiinua mgongo au posho, kadri itakavyoamuliwa na Baraza la Wawakilishi. Mshahara, malipo hayo mengineyo, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo hicho, vyote vitatokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Zanzibar na vitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(2) Mshahara na malipo mengineyo yote havitapunguzwa wakati Mwenyekiti atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

**Mwenyekiti hatashitakiwa wala kudaiwa mahakamani wakati akiwa kazini.**

**10.**—(1) Wakati wote Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, itakuwa marufuku kumshitaki au kuendesha masharti juu yake mahakamani kwa ajili ya kosa lolote la jinai.

(2) Wakati wote Mwenyekiti atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, haitaruhusu kufungua mahakamani shauri lolote la kumdai Mwenyekiti jambo lolote alilotenda au alilokosa kutenda yeye binafsi kama raia wa

kawaida ama kabla au baada ya kushika madaraka ya Mwenyekiti, ila mpaka masharti yafuatayo yawe yametimizwa kwanza, yaani—

(a) Mwenyekiti awe amepelekewa kwanza taarifa ya madai kwa maandishi angalau siku thelathini kabla ya shauri kufungu-liwa mahakamani;

(b) taarifa hiyo iwe imepelekwa kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa kufuata utaratibu ulio-wekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi;

(c) taarifa hiyo iwe imetoa maelezo kuhusu chanzo cha shauri hilo, kiini cha madai yenyewe, jina na anwani ya mahali anapoishi huyo mdai na jambo hasa analodai.

**Tafsiri.**

**11.** Katika sura hii, isipokuwa kama maelezo yahitaji vingine-vyo, "Mwenyekiti" ama "Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi" ina maana ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

## SURA YA TATU

### SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

### SEHEMU YA KWANZA

### SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Madaraka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

12.—(1) Madaraka yote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, madaraka ya Serikali yaweza kutekelezwa ama Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar mwenyewe moja kwa moja au kwa kuwakilisha madaraka hayo kwa watu wengine wenye madaraka katika utumishi wa Serikali ya Zanzibar.

(3) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Ibara hii hayazuwii sheria kukabidhi madaraka ya kutekeleza kazi kwa chombo chochote cha umma au kwa mtu mwengine yeyote ambaye si Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

### SEHEMU YA PILI

### BARAZA LA MAPINDUZI

Baraza la Mapinduzi.

13.—(1) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar ambalo wajumbe wake wasiozidi thelathini na tano watakuwa hawa wafuatao:—

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

(b) Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

(c) Wajumbe wengine.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atahudhuria mikutano ya Baraza hilo naye ndiye atakayeongoza mikutano hiyo au kama hayupo basi itaongozwa na Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi aliyeteuliwa na Mwenyekiti kwa ajili hiyo.

(3) Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mawaziri wote watateuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama ifuatavyo—

(a) kutoka miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi kutoka Tanzania Visiwani;

(b) kutoka miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Tanzania Visiwani;

(c) kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vyombo vingine vya Chama na Serikali au watu wa Tanzania Visiwani.

*Sifa za kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi.*

(4) Ili mtu aweze kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi ni lazima awe na sifa zifuatazo—

(a) awe anatimiza Miko ya Kiongozi wa Chama kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Chama cha Mapinduzi;

(b) awe anatimiza sifa za kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwakilisha Wilaya ya Uchaguzi;

(c) awe anatimiza masharti ya Uwanachama wa Kamati za Mapinduzi kwa mujibu wa Sheria ya Kamati za Mapinduzi ya 1979.

*Kazi za Baraza la Mapinduzi.*

(5) Bila ya kuingilia madaraka ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama ni Rais na Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar, Baraza la Mapinduzi litakuwa ndicho chombo Kikuu cha Kumshauri Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya mambo yote yanayohusika na utekelezaji wa madaraka yake yote ya uongozi na usimamizi juu ya shughuli za Serikali ya Zanzibar na mambo yote yasiyo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, na litamshauri Mwenyekiti juu ya mambo yoyote yatakayowasilishwa kwenye Baraza hilo kwa mujibu wa maagizo maalum au maagizo ya kawaida yatakayotolewa na Mwenyekiti.

(6) Kabla ya kuanza madaraka yake Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi hata shika madaraka yake ila mpaka awe ameapishwa kwanza kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine cho chote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

*Mawaziri.*

**14.**—(1) Kutakuwa na Mawaziri katika Baraza la Mapinduzi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar watakaoongoza Wizara ambazo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kuzianzisha mara kwa mara kwa kutoa hati maalum iliyotiwa Muhuri Rasmi wa Serikali.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atawateuwa Mawaziri na Manaibu Waziri kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ndogo ya (3) ya ibara ya 13 ya Katiba hii.

(3) Kila Waziri aliyeteuliwa atatekeleza Madaraka yake chini ya Uongozi na usimamizi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar na ataongoza Wizara au shughuli za Serikali atakazo kabidhiwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(4) Bila ya kujali masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (2), iwapo kutakuwa na haja ya kumteua Waziri au Naibu Waziri baada ya Baraza la Wawakilishi kuvunjwa, basi Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kumteuwa mtu aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi mara tu kabla Baraza la Wawakilishi halijavunjwa.

(5) Kabla ya kuanza madaraka yake Waziri au Naibu Waziri hata shika madaraka yake ila mpaka awe ameapishwa kwanza kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine cho chote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

15. Kiti cha Waziri au Naibu Waziri au Mjumbe wowote wa Baraza la Mapinduzi kitakuwa wazi litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo— Muda wa kushika Madaraka wa Memba wa Baraza la Mapinduzi na Naibu Waziri.

(a) ikiwa Mwenyekiti atamwondoa mwenye madaraka hayo kwenye kazi yake kwa kutoa hati maalum iliyotiwa Muhuri Rasmi wa Serikali; au

(b) ikiwa mwenye madaraka hayo ataacha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu yoyote ambayo haihusiki na kuvunjwa kwa Bunge au Baraza la Wawakilishi; au

(c) baada ya Mwenyekiti kukubali kujiuzulu kwa mwenye madaraka hayo; au

(d) ukiwadia wakati wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kushika madaraka yake, basi mara tu kabla Mwenyekiti hajashika madaraka.

16. Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambaye atakuwa ndiye mtendaji mkuu katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na pia Kiongozi wa Watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye atatekeleza shughuli zifuatazo kwa kufuata maagizo ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi— Katibu wa Baraza la Mapinduzi.

(a) kupanga ratiba ya mikutano ya Baraza la Mapinduzi na kutayarisha orodha ya shughuli za kila mikutano;

(b) kuandika na kuweka kumbukumbu za mikutano ya Baraza la Mapinduzi;

(c) kutoa taarifa na maelezo ya uamuzi wa Baraza kwa kila mtu anayehusika au kwa kila chombo cha umma kinachohusika.

17.—(1) Mtu yeyote aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Chama kuwa Katibu wa Chama wa Mkoa chini ya kifungu cha 56 (1) cha Katiba ya Chama atakuwa vile vile Mkuu wa Mkoa huo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ataendelea kushika madaraka ya kuwa Mkuu wa Mkoa kwa muda wote atakaokuwa Katibu wa Chama wa Mkoa. Wakuu wa Mikoa.

(2) Mkuu wa Mkoa atakuwa na madaraka ya kutekeleza katika Mkoa wake kazi na shughuli zote za Serikali ya Zanzibar zinazomhusu Mkuu wa Mkoa.

Mwanasheria Mkuu.

**18.**—(1) Kutakuwepo na Mwanasheria Mkuu atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ndiye mshauri mkuu wa Kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Licha ya kuwa mshauri Mkuu wa Kisheria kwa Serikali ya Zanzibar, Mwanasheria Mkuu pia anayo mamlaka ya uendeshaji wa mashauri yote ya jinai kwa mujibu wa sheria.

(3) Katika kutekeleza mamlaka chini ya ibara ndogo ya (2) ya kifungu hiki, mamlaka hayo yanaweza kutekelezwa na mtu mwingine katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa maagizo au kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu.

Mamlaka ya kutaja madaraka na kuwateua watu kushika madaraka.

**19.** Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo chini ya Sheria hii au masharti ya Sheria nyingine yoyote, mamlaka yafuatayo yatakuwa mikononi mwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar—

(a) mamlaka ya kuanzisha na kufuta madaraka ya namna mbali mbali katika utumishi wa Serikali ya Zanzibar:

(b) mamlaka ya kuwateua watu kushika madaraka na pia mamlaka ya kuwapandisha vyeo watu au kuwaondoa katika madaraka, kuwafukuza kazi na mamlaka ya kudhibiti nidhamu ya watu waliokabidhiwa madaraka.

Uwezo wa Kutoa Msamaha

**20.**—(1) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ana uwezo wa kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia mbele ya mahakama yoyote ya Zanzibar juu ya kosa lolote na msamaha huo unaweza kuwa na masharti au bila ya masharti kufuatana na Sheria zinazotumika Zanzibar.

(2) Msamaha unaoweza kutolewa chini ya ibara ndogo ya (1) ya ibara hii unamwezesha mtu aliyepatikana na hatia na kuadhibiwa:—

(a) kuachiliwa kabisa au kwa muda maalum; au

(b) kubadilishwa adhabu kuwa nyepesi; au

(c) kufutwa adhabu yote au sehemu ya adhabu.

## Sehemu ya Tatu

### Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi

### Baraza

Baraza la Wawakilishi.

**21.**—(1) Kutakuwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Baraza la Wawakilishi litakuwa na sehemu mbili; sehemu moja itakuwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa aina zote zilizotajwa katika Katiba hii ambao watajulikana kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi; sehemu nyingine ya Baraza la Wawakilishi itakuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Iwapo, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au masharti ya Sheria yoyote, jambo lolote linahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Baraza la Wawakilishi, basi jambo hilo halitahesabiwa kuwa limeamuliwa au limetekelezwa ipasavyo ila mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vile vile na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa madaraka yao kuhusu jambo hilo.

22.—(1) Bila kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika ibara hii, Baraza la Wawakilishi litakuwa na wajumbe wafuatao— Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(a) Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi isipokuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

(b) Wabunge wote wa kuchaguliwa na Wilaya za uchaguzi waliomo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Tanzania Visiwani;

(c) Wajumbe wawili wakuchaguliwa kutoka kila Kamati ya Mapinduzi ya Wilaya waliochaguliwa na Kamati ya Mapinduzi ya Wilaya;

(d) Wajumbe wawili wakuchaguliwa kutoka kila Kamati ya Mapinduzi ya Mkoa waliochaguliwa na Kamati ya Mapinduzi ya Mkoa;

(e) Makatibu wote wa Mikoa va Tanzania Visiwani kwa mujibu wa madaraka yao;

(f) Wajumbe wawili wa kuchaguliwa na Halmashauri Kuu ya Mkoa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa kila Mkoa;

(g) Wajumbe wawili wa Tanzania Visiwani kutoka katika kila Jumuiya inayoongozwa na Chama waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi;

(h) Wajumbe wasiozidi kumi walioteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar hatakuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

23.—(1) Ili mtu aweze kuwa mjumbe katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni lazima awe na sifa zifuatazo— Sifa za kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(a) awe raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja;

(b) awe mwanachama wa Chama anayetimiza masharti ya uwanachama kama yalivyoelezwa katika Katiba ya Chama na pia awe na sifa zifuatazo za kiongozi:—

(i) awe ni mtu aliyetosheka, na asiwe mtu aliyetawaliwa na tamaa;

(ii) awe ni mtu anayependa kueneza matunda ya Uhuru kwa wananchi wote kwa ajili ya manufaa yao na maendeleo ya Taifa kwa jumla; na

(c) awe ni mtu ambaye hakuzuiliwa kugombea uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii au kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ama Bunge la Jamhuri ya Muungano.

(2) Mtu hataweza kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi iwapo anahusika na jambo lolote kati ya mambo yafuatayo:—

(a) ikiwa mtu huyo ana uraia wa nchi nyingine yoyote;

(b) ikiwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi au Bunge la Jamhuri ya Muungano imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;

(c) ikiwa—

(i) mtu huyo amehukumiwa na Mahakama yoyote Zanzibar au katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au gerezani, kwa muda unaozidi miezi sita; au

(ii) mtu huyo amewekwa kizuizini kwa mujibu wa amri iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Kuweka kizuizini ya mwaka 1962 ya Jamhuri ya Muungano na Sheria ya 1964 ya Zanzibar na amekaa kizuizini kwa mujibu wa amri hiyo kwa muda unaozidi miezi sita; au

(iii) mtu huyo amesafirishwa kwa lazima kisheria kwa mujibu wa amri iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usafirishaji wa lazima na iwapo amekaa huko alikopelekwa kwa muda unaozidi miezi sita na mpaka wakati huo amri hiyo bado haijabatilishwa;

(d) ikiwa mtu huyo ana masilahi yoyote katika mkataba wa Serikali wa aina yoyote iliyowekwa miiko maalum kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na iwapo amekiuka miiko hiyo;

(e) ikiwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi mtu huyo amezuiliwa kuwa mjumbe katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu kwamba ameshika madaraka katika utumishi wa Serikali ya Zanzibar na Sheria hiyo imetamka wazi kuwa ni mwiko kwa mtu huyo kuwa mjumbe katika Baraza la Wawakilishi;

(f) ikiwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia makosa yanayohusika na uwakilishi wa aina yoyote mtu huyo amezuiliwa kuwa mwakilishi;

(g) ikiwa mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, ana hisa au masilahi mengineyo yoyote ya aina hiyo katika kampuni yoyote;

(h) ikiwa mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, ni Mkurugenzi katika Kampuni yoyote ya kibepari au ya kikabaila;

(i) ikiwa mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, ana nyumba ya kupangisha;

(j) ikiwa mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, hupata riziki yake kwa kuajiri watu wengine:

Isipokuwa kwamba mtu huyo hatahesabiwa kuwa amepoteza sifa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa mtu huyo anamwajiri mtu mwingine kwa ajili ya kufanya kazi za msimu na huyo mtu alieajiriwa hulipwa kwa kutwa kwa kufuata muda aliofanya kazi au kazi maalum aliyofanya.

(3) Mtu hataweza kugombea kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa wakati huo yeye ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(4) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomzuia mtu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi muda wowote utakaotajwa na Baraza la Wawakilishi (ili mradi muda huo usizidi miaka mitano) ikiwa mtu huyo atapatikana na hatia mbele ya mahakama kwa ajili ya aina yoyote ya makosa yatakayotajwa katika Sheria hiyo yanayohusika na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(5) Kwa madhumuni ya kutoa fursa ya kukata rufaa kwa mujibu wa Sheria kwa mtu yeyote aliyethibitishwa rasmi kisheria kuwa na ugonjwa wa akili au aliyehukumiwa na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au Gerezani aliepatikana na hatia ya kosa lolote lililotajwa katika Sheria kwa mujibu wa ibara ndogo ya (4) ya ibara hii. Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayoeleza kwamba hiyo hukumu inayopingwa na mtu huyo haitakuwa na nguvu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya ibara ndogo ya (2) au ya (4) ya ibara hii mpaka upite kwanza muda utakaotajwa katika Sheria hiyo.

(6) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (c) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, yaani—

(a) ikiwa mtu amepewa adhabu mbili au zaidi za kufungwa Chuo cha Mafunzo au gerezani na ameamriwa afungwe kwa muda wa mfululizo, basi adhabu hizo zitahesabiwa kuwa ni adhabu mbali mbali iwapo muda uliotajwa katika kila moja ya adhabu hizo hauzidi miezi sita, lakini iwapo muda uliotajwa katika adhabu yoyote kati ya adhabu hizo unazidi miezi sita basi adhabu hizo zote zitahesabiwa kama ni adhabu moja;

(b) ikiwa mtu amepewa adhabu ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au gerezani ikifahamika kuwa adhabu hiyo ya kifungo imetolewa badala ya adhabu ya kutozwa faini au imetolewa kwa sababu mtu huyo ameshindwa kulipa faini aliyoamriwa kulipa, basi muda wa kifungo cha namna hiyo hautahesabiwa.

(7) Katika aya ya (d) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, "mkataba wa Serikali" maana yake ni mapatano yoyote ya mkataba ambayo mmoja wapo wa walioshiriki ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au idara yoyote ya Serikali au mtumishi yeyote wa Serikali aliyeshiriki kwa niaba ya Serikali.

(8) Kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (g) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, "hisa" ifahamike kwa maana ya kawaida ya neno hilo na vile vile ni pamoja na hati ya dhamana au ya aina ya stakabadhi ya fedha iliyowekwa akiba au iliyokopeshwa, na pia faida au mali nyingineyo yoyote.

(9) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (g) ama aya ya (i) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, yaani—

(a) mtu hatahesabiwa kuwa ana hisa katika kampuni au kuwa ana nyumba ya kupangisha au kuwa ana maslahi mengineyo yoyote katika kampuni yoyote au nyumba yoyote ikiwa mali au maslahi aliyonayo amepata kutokana na mali waliyoshikia wadhamini kwa niaba yake au amepata kwa mujibu wa masharti ya wakf na ikiwa—

(i) yeye mwenyewe hakuwa miongoni mwa wale watu waliofanya mipango ya kukabidhi mali kwa wadhamini wala mipango ya kuweka wakf; na

(ii) iwapo mali au maslahi aliyo nayo amepata baada ya siku ya kwanza tangu kuwa Mjumbe Mwakilishi lakini kabla ya mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, kushika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi, basi mtu huyo awasilishe kwenye Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Visiwani tamko rasmi katika fomu maalum itakayotumiwa kwa ajili hiyo kwamba ataondokana na mali hiyo au maslahi hayo kabla ya kumalizika miezi mitatu tangu siku ambayo mtu huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, atakavyoshika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi.

(10) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (j) ya ibara ndogo ya (2), yaani—

(a) "mshahara" maana yake ni—

(i) malipo yanayotolewa kwa mtu kama ujira wake kwa ajili ya kazi anazotekeleza kama Mjumbe Mwakilishi, lakini siyo pamoja na posho yoyote anayolipwa kama Mjumbe Mwakilishi;

(ii) mapato yanayotokana na shughuli zake kama mkulima au kama mfanyakazi;

(iii) ujira anaolipwa mtu kwa mujibu wa mapatano ya mkataba wa kazi;

(iv) mali anayopata mtu kutoka kwa wadhamini wanaoshikilia mali kwa niaba yake kwa mujibu wa dhamana au wakf;

(b) ikiwa mtu anapokea mishahara miwili au zaidi, basi atahesabiwa kuwa anapokea mshahara mmoja tu iwapo jumla ya fedha yote anayopokea haizidi kiwango cha mshahara anaolipwa Mjumbe Mwakilishi;

(c) mtu yeyote anayepokea mshahara hatapoteza sifa za kugombea kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa sababu tu kwamba akichaguliwa ataendelea kupokea mshahara wake na vile vile atakuwa na haki ya kulipwa mshahara kama Mjumbe Mwakilishi; lakini mtu huyo atalazimika, kabla ya kushika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi kuwasilisha kwa Spika tamko rasmi katika fomu maalum itakayotumiwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria hii kwamba—

(i) ataacha kupokea mmoja wapo wa mishahara hiyo miwili; au

(ii) atapokea sehemu tu ya mshahara anaostahili kulipwa kama Mjumbe Mwakilishi ili kwamba sehemu hiyo ikichanganywa na ule mshahara wake mwingine jumla ya fedha yote haitazidi kiwango cha mshahara anaolipwa Mjumbe Mwakilishi; na

(11) Kwa ajili ya ufafanuzi wa maelezo kuhusu sifa za uchaguzi yaliyomo katika ibara zifuatazo, kila itakapotajwa chini ya Katiba hii kwamba utekelezaji wa jambo lolote wahitaji mtu mwenye sifa za uongozi au mtu ambaye hakupoteza sifa za uongozi, basi, ila iwapo maelezo yahitajia vinginevyo, ifahamike kuwa sifa zinazohusika ni zile zinazomwezesha mtu kuchaguliwa kuwa Mjumbe Mwakilishi au Baraza la Mapinduzi kama viongozi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoeleza katika vifungu mbali mbali vya Katiba hii miongoni mwao ikiwa—

(a) Ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliyopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi, au kwa upendeleo, au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa madaraka hayo;

(b) ni mwiko kwa kiongozi kupokea kipato cha kificho, au rushwa, au kushiriki katika mambo yo yote ya magendo; na

(c) kiongozi aliyeachishwa uongozi hatakuwa na haki ya kuomba tena nafasi ya uongozi mpaka ipite miaka mitano tangu alipoachishwa hivyo.

**24.** Kila Mjumbe Mwakilishi atatakiwa kuapishwa, katika Baraza la Wawakilishi, kiapo cha uaminifu kabla hajaanza kushiriki katika shughuli za Baraza la Wawakilishi; lakini Mjumbe Mwakilishi anaweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika hata kabla hajaapishwa.

**Kiapo cha Mjumbe Mwakilishi.**

**25.**—(1) Kila Mjumbe Mwakilishi atatakiwa, kabla ya kumaliza siku kumi na tano tangu ashike madaraka katika Baraza la Wawakilishi kama Mjumbe Mwakilishi, kuwasilisha kwa Spika nakala mbili za tamko rasmi kwamba yeye hajapoteza sifa za kuendelea kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa chini ya Katiba hii kama sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi.

**Tamko Rasmi la Wajumbe Wawakilishi kuhusu Masharti ya Uongozi.**

(2) Tamko rasmi linalotakiwa kuwasilishwa kwa Spika kwa mujibu wa masharti ya ibara hii litatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayowekwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(3) Masharti ya ibara hii yatatumika kwa kila Mjumbe Mwakilishi, isipokuwa Mkuu wa Mkoa.

(4) Spika atawasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi nakala moja ya kila tamko rasmi lililowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(5) Katika ibara hii na katika ibara nyingine katika Katiba hii "Tume ya Tabia ya Viongozi" maana yake ni Tume iliyotajwa katika ibara ya 61 ya Katiba hii.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoa taarifa ya mali.

26.—(1) Kila Mjumbe Mwakilishi anayehusika na masharti ya ibara hii atatakiwa kuwasilisha kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali yake na, kadri itakavyokuwa, mali ya mke wake au mume wake. Taarifa hiyo itatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayotumika maalumu kwa kazi hiyo kwa mujibu wa Katiba hii.

(2) Masharti ya ibara hii yatatumika kwa kila Mjumbe Mwakilishi, isipokuwa Mkuu wa Mkoa.

(3) Spika atawasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi nakala moja ya kila taarifa rasmi iliyowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(4) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kwa makusudi ya kuhifadhi kama siri kila taarifa ya mali iliyowasilishwa na Mjumbe Mwakilishi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, na masharti hayo yaweza kueleza mambo yafuatayo:—

(a) kwamba taarifa ya mali yaweza kutolewa tu ikiwa inahitajiwa kama ushahidi mbele ya Mahakama Kuu wakati inaposikiliza shauri lililofunguliwa katika Mahakama Kuu kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuhusu masharti ambayo Mahakama Kuu ina mamlaka kusikiliza juu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(b) kwamba kabla taarifa ya mali haijatolewa kama ushahidi mbele ya Mahakama Kuu, watu pekee wanaoweza kuona taarifa hiyo au kujua yaliyomo katika taarifa hiyo ni wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi, Wajumbe wa Tume ya Tabia ya Viongozi, watumishi wa Tume ya Tabia ya Viongozi, na wakuu wengine walioruhusiwa kwa mujibu wa Sheria hiyo;

(c) mambo mengine yoyote ambayo yatahakikisha kwamba watu wasioruhusiwa au wasiohusika hawapati nafasi ya kuona taarifa ya mali wala kujua yaliyomo katika taarifa ya mali.

**27.**—(1) Mjumbe Mwakilishi ataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi na ataacha kiti chake katika Baraza la Wawakilishi litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo— Muda wa Wajumbe Wawakilishi kushika madaraka yao.

(a) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe Mwakilishi, lingemfanya asiwe na sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi au kuwa kiongozi kwa mujibu wa ufafanuzi wa Katiba hii na Katiba ya Chama:

Isipokuwa kwamba iwapo Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, amepata mali au masilahi menginevo voyote yaliyotokana na haki ya kumiliki hisa katika kampuni au haki ya kumiliki nyumba na ikiwa mali au maslahi hayo amepata kwa njia ya urithi, au kwa mujibu wa Sheria, basi Mjumbe Mwakilishi huyo hataacha kiti chake katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu ya masharti yaliyowekwa chini ya Katiba hii kama Mjumbe Mwakilishi huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, atachukua hatua za kuondokana na mali au maslahi hayo kabla ya kumalizika miezi mitatu tangu mali hiyo au maslahi hayo yalipopatikana.

(b) ikiwa Mjumbe Mwakilishi huyo atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar;

(c) kwa Mjumbe Mwakilishi asiye Mkuu wa Mkoa, ikiwa atakosa kuhudhuria vikao vya Mikutano ya Baraza la Wawakilishi vitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Spika;

(d) iwapo Mjumbe Mwakilishi, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, ametoa tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuhusu sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi katika Baraza la Wawakilishi, basi ikiwa Mjumbe Mwakilishi huyo, au kadri itakavyokuwa, mke wake au mume wake, atashindwa kutimiza yaliyomo katika tamko hilo;

(e) kwa Mjumbe Mwakilishi ambaye anatakiwa kutoa tamko rasmi kuhusu masharti ya uongozi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, ikiwa litatokea lolote kati ya mambo yafuatayo:—

(i) ikiwa atashindwa kutoa hilo tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii katika muda uliowekwa mahsusi kwa ajili hiyo; au

(ii) ikiwa atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uwongo kwa kiapo, kinyume na Sheria ya Kanuni za Jinai, kuhusu hilo tamko rasmi;

(f) kwa Mjumbe Mwakilishi anatakiwa kutoa taarifa rasmi ya mali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, ikiwa atashindwa kutoa hilo tamko rasmi katika muda uliowekwa mahususi kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, lakini iwapo Mjumbe Mwakilishi hataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa mujibu wa jambo

lolote kati ya mambo hayo yaliyotajwa na kama hatajiuzulu au kufariki mapema zaidi, basi Mjumbe Mwakilishi ataendelea kushika madaraka yake kama Mjumbe Mwakilishi mpaka Baraza la Wawakilishi litakapovunjwa.

(2) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomwezesha Mjumbe Mwakilishi kukata rufaa, kwa mujibu wa Sheria kupinga hukumu ya kuthibitishwa kwake kuwa ni mtu mwenye ugonjwa wa akili, au kupinga adhabu ya kifo au ya kufungwa Chuo cha Mafunzo au gerezani au kupinga kupatikana kwake na hatia kwa kosa la aina iliyotajwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 23 ya Katiba hii au kosa la kutoa habari za uwongo kwa kiapo, kinyume na Sheria ya Kanuni za Jinai, kuhusu tamko rasmi lililotolewa kwa mujibu wa masharti ya aya ya (f) ya ibara ndogo (1) ya ibara hii, na Sheria hiyo yaweza kueleza kwamba hiyo hukumu inayopingwa na huyo Mjumbe Mwakilishi haitatiliwa nguvu kisheria mpaka umalizike kwanza muda utakaotajwa katika Sheria hiyo.

Uamuzi wa Suala kama mtu ni Mjumbe Mwakilishi ama sio.

**28.**—(1) Mahakama Kuu ya Zanzibar ndiyo pekee yenye mamlaka ya kusikiliza shauri na kuamua suala kuhusu mambo yafuatayo:—

(a) kama uteuzi wa mtu yeyote kuwa Mjumbe Mwakilishi ulikuwa halali au sivyo; au

(b) kama Mjumbe Mwakilishi amekoma kuwa Mjumbe Mwakilishi na kiti chake katika Baraza la Wawakilishi ki wazi au hapana:

Isipokuwa kwamba iwapo Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara ya 6 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imemtangaza Mjumbe Mwakilishi yeyote kwamba amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano au Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Visiwani imemtangaza Mjumbe Mwakilishi yeyote kuwa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar, basi Mahakama Kuu haitachunguza zaidi suala lolote linalohusu kiti cha Mjumbe Mwakilishi huyo kuwa wazi.

(2) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo:—

(a) watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala lolote kwa mujibu wa masharti ya ibara hii;

(b) sababu na nyakati za kufungua shauri la namna hiyo, utaratibu wa kufungua shauri na masharti yanayotakiwa yatimizwe kwa kila shauri kama hilo; na

(c) kutaja mamlaka ya Mahakama Kuu juu ya shauri la namna hiyo, na kueleza utaratibu wa kusikiliza shauri lenyewe.

(3) Uamuzi wa Mahakama Kuu juu ya shauri lolote lililosikilizwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii utakuwa wa mwisho; hakutakuwa na haki ya kukata rufaa popote kupinga uamuzi huo.

29.—(1) Kutakuwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atachaguliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa watu ambao ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au wenye sifa za uchaguzi. Spika.

(2) Memba wa Baraza la Mapinduzi, Naibu Waziri au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote itakayotajwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya ibara hii, hataweza kuchaguliwa kuwa Spika.

(3) Mtu ambaye atakuwa ameshika madaraka ya Spika kwa mujibu wa ibara ndogo (1) ya kifungu hiki atatakiwa kuwasilisha kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar nakala mbili za tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa zinazotakiwa kuwa Mjumbe Mwakilishi kabla ya siku kumi na nne kumalizika tangu kuchaguliwa kwake. Tamko hilo litatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayowekwa kwa mujibu wa Katiba hii.

(4) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atawasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume ya Tabia ya Viongozi nakala moja ya kila tamko rasmi lililowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii.

(5) Spika atatakiwa kuwasilisha kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali ya huyo Spika na kadri itakavyokuwa, mali ya mke wake au mume wake. Spika atatoa taarifa hiyo kwa kutumia fomu maalum iliyowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na atatoa taarifa ya namna hiyo mara kwa mara kadri itakavyoagiza Sheria hiyo.

(6) Spika ataacha kuwa Spika na ataacha kiti cha Spika litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:—

(a) iwapo mtu huyo alichaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi ikiwa ataacha kuwa Mjumbe Mwakilishi kwa sababu yoyote ambayo haihusiki na kuvunjwa Baraza la Wawakilishi; au

(b) ikiwa kutatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Spika, lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za kuwa Mjumbe Mwakilishi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika; au

(c) ikiwa mtu huyo ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa azimio la Baraza la Wawakilishi lililoungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote; au

**33.**—(1) Baraza la Wawakilishi litafanya mikutano yake mahali ambapo ni desturi kufanya Mikutano hiyo au mahali pengine popote Zanzibar patakapotajwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili hiyo. Mikutano ya Baraza la Wawakilishi.

(2) Mkutano wa kwanza wa Baraza la Wawakilishi katika Maisha ya Baraza la Wawakilishi utaanza siku ile ambayo Baraza la Wawakilishi jipya limeitwa kukutana, na kila Mkutano ufuatao utaanza siku yoyote itakayopangwa na Baraza la Wawakilishi lenyewe au siku yoyote itakayopangwa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

(3) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wakati wowote.

**34.**—(1) Kila kikao cha Baraza la Wawakilishi kitaongozwa na mmoja wapo wa watu wafuatao yaani— Uongozi wa Vikao vya Baraza la Wawakilishi.

(a) Spika;au

(b) Ikiwa Spika hayupo,
Kaimu Spika.

**35.** Kiwango cha kila kikao cha Baraza la Wawakilishi ni nusu ya Wawakilishi wote. Kiwango cha Vikao vya Baraza la Wawakilishi.

**36.**—(1) Isipokuwa kama imeelezwa vingine katika Katiba hii, kila suala litakalotolewa kwa ajili ya kupata uamuzi wa Baraza la Wawakilishi litaamuliwa kwa kufuata wingi wa kura za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliohudhuria na kupiga kura. Kiwango cha kura katika kufikia uamuzi katika Baraza la Wawakilishi.

(2) Spika, au Kaimu Spika hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi kukitokea usawa wa kura.

(3) Kanuni za Baraza la Wawakilishi zaweza kuweka masharti kwamba Mjumbe Mwakilishi yeyote atakayepiga kura juu ya jambo lolote ambalo yeye binafsi ana masilahi nalo atahesabiwa kuwa hakupiga kura.

**37.**—(1) Kutakuwa na Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi zifuatazo— Kamati ya Baraza la Wawakilishi.

(a) Kamati ya Fedha ya Uchumi;

(b) Kamati ya Mambo ya Siasa;

(c) Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali;

(d) Kamati ya Mambo ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii;

(e) Kamati ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi; na

(f) Kamati ya Mambo Mengineyo.

(2) Baraza la Wawakilishi laweza kuunda Kamati nyingine za namna mbali mbali kadiri litakavyoona inafaa.

(3) Kamati za Bazara la Wawakilishi zaweza kuweka utaratibu wa kuunda Kamati za Baraza la Wawakilishi na kueleza kazi za kila Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kuhutubia Baraza la Wawakilishi

**38.** Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza wakati wowote kulihutubia Baraza la Wawakilishi au kupeleka kwenye Baraza la Wawakilishi Taarifa ambayo itasomwa na Waziri.

Viti vilivyowazi katika Baraza la Wawakilishi na utaratibu wakuendesha shughuli za Baraza la Wawakilishi.

**39.**—(1) Baraza la Wawakilishi laweza kutekeleza shughuli wakati wa vikao vyake bila ya kujali kwamba kuna kiti kilicho wazi miongoni mwa viti vya wawakilishi na iwapo katika shughuli hizo atashiriki mtu yeyote ambaye hana haki ya kushiriki au kama wakati wa shughuli hizo atakuwapo mtu yeyote ambaye hana haki ya kuwapo, basi kushiriki kwa mtu huyo au kuwapo kwake hakutabadilisha shughuli hizo.

(2) Baraza la Wawakilishi laweza, lakini bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, kuweka Kanuni za utaratibu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake.

Madaraka ya Sheria.

**40.** Madaraka yote ya kutunga Sheria katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyokuwa ya Muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

Utaratibu wa kutunga Sheria.

**41.**—(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii, Baraza la Wawakilishi litatumia madaraka yake ya kutunga Sheria kwa kufuata utaratibu wa kujadili na kupitisha miswada ambayo hatimaye itabidi ipate kibali cha Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar, na Muswada hautakuwa Sheria mpaka uwe umepitishwa na Baraza la Wawakilishi na kukubaliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(2) Baada ya Muswada kuwakilishwa kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili ya kupata kibali chake, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza ama kukubali au kukataa kuukubali, na iwapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atakataa kuukubali Muswada, basi atauridisha Baraza la Wawakilishi pamoja na maelezo ya sababu zake za kukataa kuukubali Muswada huo.

(3) Baada ya Muswada kurudishwa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, hauwezi kupelekwa tena kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili ya kupata kibali chake kabla ya kumaliza muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, isipokuwa kama katika hatua yake ya mwisho kwenye Baraza la Wawakilishi kabla haujapelekwa tena

kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar Muswada huo umeungwa mkono na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote.

(4) Iwapo Muswada umerudishwa Baraza la Wawakilishi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar, halafu ukaungwa mkono kwenye Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (3) na kupelekwa kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili ya kupata kibali chake kwa mara ya pili kabla haujamalizika muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, basi Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais ya Zanzibar atatakiwa kuukubali Muswada huo kabla ya kumalizika muda wa siku ishirini na moja tangu Muswada huo ulipowasilishwa kwake, la sivyo basi itabidi alivunje Baraza la Wawakilishi.

(5) Masharti yaliyomo katika ibara hii au katika ibara ya 40 ya Katiba hii hayatalizuia Baraza la Wawakilishi kutunga Sheria na kuweka Masharti ambayo yaweza kukabidhi kwa mtu yeyote au kwa Idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali.

**Masharti ya kubadilisha Katiba hii.**

**42.**—(1) Ili kuweza kubadilisha masharti yoyote ya Sheria hii ambayo ni msingi wa Katiba ya Serikali ya Zanzibar, muswada wa Sheria inayoleta mabadiliko hayo ni lazima uungwe mkono kwa kura za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasiopungua robo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote.

(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (1), kubadilisha masharti ya Sheria maana yake ifahamike kuwa ni pamoja na kurekebisha au kusahihisha masharti hayo au kufuata na kuweka masharti mengine badala yake au kusisitiza au kubadilisha matumizi ya masharti hayo.

**Uhusiano kati ya Baraza la Wawakilishi na Chama.**

**43.**—(1) Baraza la Wawakilishi ni Kamati ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama, kwa mujibu wa ibara ndogo ya (12) ya ibara ya 59 ya Katiba ya Chama ambayo kazi yake ni kusimamia kwa ujumla utekelezaji wa siasa ya Chama katika shughuli zote zinazoendeshwa na Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Pamoja na kutumia njia nyingine za kutekeleza shughuli zake kama ilivyoelezwa katika Katiba hii, Baraza la Wawakilishi litatekeleza kazi yake iliyoelezwa katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hii kwa njia zifuatazo:—

(a) kwa kuiuliza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar maswali mbali mbali kwenye Baraza la Wawakilishi.

(b) Kwa kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa kila mwaka wa Makisio ya Matumizi; na

(c) kwa kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo Sheria.

## SURA YA NNE

### MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR, TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA YA ZANZIBAR, BARAZA LA JUU NA UTARATIBU WA KUPELEKA HATI NA KUTEKELEZA MAAGIZO YALIYOMO KATIKA HATI ZILIZOTOLEWA NA MAHKAMA

### SEHEMU YA KWANZA

**44.**—(1) Kutakuwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar ambayo mamlaka yake yatakuwa kama ilivyoelezwa katika Katiba hii au katika Sheria nyingine yoyote. **Mahakama Kuu ya Zanzibar.**

(2) Kutakuwa na Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu ya Zanzibar na Majaji wengine wa Mahakama Kuu kwa idadi ambayo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ushauriano na Jaji Mkuu ataona inahitajika.

(3) Kazi ya Jaji haitafutwa wakati yupo mtu aliyeshika madaraka ya kiti cha Jaji.

(4) Isipokuwa kama Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi itaagiza vyengine, Mahakama Kuu ya Zanzibar itakuwa na uwezo wa kutekeleza shughuli zote ambazo kwa kawaida huambatana na mahakama yenye hadhi kama hiyo.

**45.**—(1) Jaji Mkuu wa Zanzibar atateuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar. **Uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu.**

(2) Majaji wengine wa Mahakama Kuu ya Zanzibar watateuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar baada ya kushauriana na Jaji Mkuu wa Zanzibar.

(3) Mtu aweza tu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar ikiwa ana sifa zifuatazo:—

(a) awe na shabaha ya Sheria ya Chuo Kikuu kinachotambulika; na

(b) awe amefanya kazi inayohusika na Sheria na kupata uzoefu wa muda usiopungua miaka mitano.

(4) Iwapo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atatosheka kwamba japokuwa mtu mwenye sifa kama ilivyoelezwa katika aya (a) ya ibara ndogo (3) ya Ibara hii hakuwa nayo sifa hiyo kwa muda usiopungua miaka mitano, lakini mtu huyo ana uwezo, ujuzi na kwa kila hali anafaa kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar na kuna sababu maalum za kumfanya mtu huyo astahiki kukabidhiwa madaraka hayo, basi Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kutengua lile sharti la kuwa na sifa hiyo kwa muda usiopungua miaka mitano, na baada ya kushauriana na Jaji Mkuu kama kawaida Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kumteua mtu huyo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

(5) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji Mkuu kitakuwa wazi au kwamba Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, basi kazi hizo zitatekelezwa na Jaji mmoja wapo atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili hiyo kama Kaimu Jaji Mkuu na Jaji huyo atatekeleza kazi hizo mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwengine na kushika madaraka ya kiti cha Jaji Mkuu au mpaka Jaji Mkuu mwenyewe ambae alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.

Muda wa Kushika Madaraka wa Majaji.

46.—(1) Kila Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka hamsini na tano, lakini masharti ya ibara hii ndogo yatatumika bila ya kuathiri masharti yafuatayo katika ibara hii.

(2) Jaji yeyote wa Mahakama Kuu ya Zanzibar aweza kujiuzulu kazi katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wowote baada ya kutimiza umri wa miaka arobaini na tano isipokuwa kama Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ataagiza kwamba asijiuzulu, na iwapo itaagizwa hivyo, basi huyo Jaji atakayehusika na maagizo hayo ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar hatakuwa na haki ya kujiuzulu mpaka upite kwanza muda wowote utakaotajwa katika maagizo hayo.

(3) Iwapo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ataona kuwa kwa ajili ya manufaa ya Umma inafaa Jaji aliyetimiza umri wa miaka hamsini na tano aendelee kufanya kazi, na huyo Jaji mwenyewe anakubali kwa maandishi kuendelea kufanya kazi, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kuagiza kuwa Jaji huyo aendelee kufanya kazi kwa muda wowote utakaotajwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(4) Bila ya kujali kwamba Jaji ametimiza umri ambao analazimika kuacha kazi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, mtu anayefanya kazi ya Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar aweza kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri huo mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na masharti ambayo alikwisha anza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri huo wa kuacha kazi.

(5) Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi ya Jaji kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na sababu nyengine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa mashauri ya ibara ndogo ya (7) ya ibara hii.

(6) Iwapo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar anaona kuwa suala la kumwondoa Jaji kazini lahitaji kuchunguzwa basi katika hali hiyo mambo yatakuwa ifuatavyo:—

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atateua Tume Maalum ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili. Huyo Mwenyekiti

wa Tume hiyo itabidi awe mtu ambaye ni Jaji, au mtu aliyepata kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na Wajumbe wengine wenye sifa nzuri za uongozi watatoka Serikalini na kwenye Chama;

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kama huyo Jaji anayehusika aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(7) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (6) itamshauri Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwamba Jaji ambaye habari zake zimechunguzwa na hiyo Tume aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atamwondoa kazini Jaji huyo anayehusika.

(8) Ikiwa suala la kumwondoa Jaji kazini limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (6) ya ibara hii, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kumsimamisha kazi Jaji huyo anayehusika, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza wakati wowote kufuta uamuzi huo wa kumsimamisha kazi Jaji huyo, na kwa hali yoyote uamuzi huo utaachiwa, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa busara yake ikiwa Tume itamshauri Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwamba Jaji huyo asiondolewe kazini.

(9) Masharti ya ibara hii yatatumika bila ya kuathiri masharti ya vifungu vingine vya Sheria hii.

Kiapo cha Majaji.

**47.** Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar hatashika madaraka yake ila mpaka awe ameapishwa kwanza kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi kitakachowekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

**48.** Bila ya kuathiri masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 au ya Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, iwapo Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Muungano juu ya mambo ya Muungano inayotumika Tanzania Bara na vile vile Tanzania Visiwani imekabidhi madaraka yoyote kwa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, basi Mahakama Kuu ya Zanzibar yaweza kutekeleza madaraka hayo kwa kiasi kile kile inavyoweza kutekeleza Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano.

## SEHEMU YA PILI

## MADARAKA YA KUAJIRI MAHAKIMU NA WATUMISHI WENGINE WA MAHAKAMA ZA ZANZIBAR NA TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA.

Tume ya Kuajiri ya Mahakama.

**49.**—(1) Kutakuwa na Tume ya kuajiri kwa ajili ya Mahakimu na Watumishi wengineo wa Mahakama za Zanzibar. Wajumbe wa Tume hiyo watakuwa hawa wafuatao—

(a) Jaji Mkuu wa Zanzibar, ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Jaji mmoja wa Mahakama Kuu ya Zanzibar ambaye atateuliwa kwa ajili hiyo na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar baada ya kushauriana na Jaji Mkuu;

(c) Mjumbe mmoja ambaye atateuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(2) Mtu hataweza kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume kwa mujibu wa masharti ya aya ya (c) ya ibara ndogo ya (1) ya ibara hii ikiwa mtu huyo ni Mjumbe Mwakilishi au ni mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote iliyotajwa kwa ajili hiyo na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Madaraka ya Kuajiri Mahakimu na Watumishi wengineo wa Mahakama.

**50.**—(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inayohusika na suala la kuajiri Mahakimu na Watumishi wengineo wa Mahakama, mgawano wa madaraka kwa ajili ya suala hilo utakuwa ifuatavyo—

(a) madaraka ya kuwaajiri watu wa kushika madaraka ya aina zilizotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii (pamoja na madaraka ya kuwathibitisha watu hao kazini na kuwapandisha vyeo) yatakuwa mikononi mwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar;

(b) madaraka ya kudhibiti nidhamu ya watu hao na madaraka ya kuwaondoa kazini yatakuwa mikononi mwa Tume ya Kuajiri ya Mahakama iliyotajwa katika ibara ya 49 ya Katiba hii, kwa ridhaa ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(2) Madaraka yanayohusika na masharti ya ibara hii ni madaraka ya Mrajis wa Mahakama Kuu ya Zanzibar na madaraka ya Mahakimu ya aina nyengine yoyote, na madaraka ya aina nyingine yoyote yanayohusika na Mahakama yoyote itakayotajwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

## SEHEMU YA TATU

## BARAZA LA JUU

**51.**—(1) Kutakuwa na Baraza la Juu la Zanzibar ambalo mamlaka yake yatakuwa kama ilivyoelezwa katika Katiba hii au katika Sheria nyingine yoyote.

(2) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Baraza la Juu na wajumbe wengine wa Baraza la Juu kwa idadi ambayo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar ataona inahitajiwa.

Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza la Juu.

**52.** Mwenyekiti wa Baraza la Juu na Wajumbe wote wa Baraza la Juu watateuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

Kazi za Baraza la juu.

**53.** Baraza la Juu litasikiliza na kuamua rufaani kutokana na uamuzi wa Mahkama Kuu ya Zanzibar na mashauri yatakayofikishwa mbele yake kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Juu, 1970.

Mahakama ya Rufaani ya Tanzania.

**54.** Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga Sheria ya kuwezesha kupeleka rufaani kutoka Mahkama Kuu ya Zanzibar au Baraza la Juu kusikilizwa katika Mahkama ya Rufaani ya Tanzania iliyoundwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

## Sehemu ya Nne

## Utaratibu wa Kupeleka Hati na Kutekeleza Maagizo Yaliyomo Katika Hati Zilizotolewa na Mahakama

Utekelezaji wa Maagizo ya Mahakama Utafanywa nchini Tanzania kote.

**55.**—(1) Hati zenye maagizo yaliyotolewa na Mahakama za Tanzania Bara na Mahakama za Tanzania Visiwani katika masharti ya madai ya aina zote na mashauri ya jinai ya aina zote (pamoja na hati za kuamuru kukamata watu) zaweza kupelekwa mahali popote nchini Tanzania na maagizo hayo yaweza kutekelezwa mahali popote nchini Tanzania kwa kufuata masharti yafuatayo—

(a) iwapo Mahakama imetoa hati yenye maagizo yatakayotekelezwa mahali ambako Mahakama hiyo haina mamlaka, basi hati hiyo itapelekwa huko na maagizo yaliyomo katika hati hiyo yatatekelezwa kwa mujibu wa utaratibu unaotumika huko kwa ajili ya kupeleka hati au kutekeleza maagizo yaliyomo katika hati iliyotolewa na Mahakama yenye mamlaka huko ilikopelekwa hati; na

(b) iwapo sheria inayotumika huko ilikopelekwa hati imeweka masharti kwamba hati zilizotolewa na Mahakama ya mahali pengine ni lazima ithibitishwe kwanza na Mahakama yenye mamlaka mahali hapo inapotumika Sheria hiyo, basi kila hati iliyotolewa na Mahakama ya mahali pengine itabidi ithibitishwe kwanza kwa mujibu wa Sheria hiyo kabla maagizo yaliyomo katika hati hiyo hayajatekelezwa.

(2) Iwapo mtu amekamatwa mahali popote nchini Tanzania kwa mujibu wa hati ya kuamuru kukamatwa kwake iliyotolewa na Mahakama ambayo haina mamlaka mahali hapo alipokamatwa mtu huyo, basi mtu huyo atahesabiwa kuwa yuko chini ya ulinzi halali na aweza kufikishwa mbele ya Mahakama iliyotoa hati hiyo,

lakini masharti haya yaliyomo katika ibara hii ndogo itabidi yatumiwe bila kuathiri masharti ya Serikali inayotumika hapo mahali alipokamatwa mtu huyo.

(3) Masharti yaliyomo katika ibara hii hayatazuia Sheria kuweka utaratibu kwa ajili ya kupeleka nje ya Tanzania hati zilizotolewa na Mahakama za Tanzania Bara au Mahakama za Tanzania Visiwani.

## SURA YA TANO

### MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

**56.** Mahakama maalumu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa ibara ya 71 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977, itatekeleza shughuli zake Tanzania Visiwani kufuatana na utaratibu wa Kisheria uliowekwa kwa mujibu wa ibara za 72, 73 na 74 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977. Mahakama maalumu ya Jamhuri ya Muungano.

## SURA YA SITA

### Baraza la Mipango

Baraza la Mipango.

**57.** Kutakuwa na Baraza la Mipango katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambalo ndiyo chombo kikuu kinachoandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii kwa upande wa Tanzania Visiwani.

Wajumbe wa Baraza la Mipango.

**58.**—(1) Baraza la Mipango litakuwa na Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti na Wajumbe wengine kama ifuatavyo:—

(a) Wajumbe wote wa Baraza la Mapinduzi;

(b) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi;

(c) Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka Tanzania Visiwani;

(d) Wajumbe wa Kamati Tendaji za Mikoa na Wilaya;

(e) Wajumbe wanne watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi watakaowakilisha baadhi ya Wizara, na Mashirika ya Umma ya Zanzibar;

(f) Mjumbe mmoja kutoka kila Jumuiya ya Chama watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

Mikutano ya Baraza la Mipango.

(2) Baraza la Mipango litakuwa likikutana mara moja kila mwaka ili kuzingatia mipango ya muda mrefu na ya muda mfupi.

Mwenyekiti.

(3) Mwenyekiti wa Mikutano ya Baraza la Mipango atakuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

Tume ya Kudumu ya Mipango.

**59.** Kutakuwa na Tume ya Kudumu ya Baraza la Mipango ya Zanzibar ambayo itakuwa ni chombo cha utekelezaji cha Baraza la Mipango. Utaratibu wa kutekeleza shughuli za Tume pamoja na muundo wake utakuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi au sheria nyingine inayohusika Zanzibar.

## SURA YA SABA

### SEHEMU YA KWANZA

### TUME YA KUDUMU YA UCHUNGUZI

**60.** Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ya Jamhuri ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 itakuwa na mamlaka ya kutekeleza shughuli zake Tanzania Visiwani kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Sheria yoyote itakayotungwa chini ya Katiba hiyo na Bunge au na Baraza la Wawakilishi. Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.

### SEHEMU YA PILI

### TUME YA TABIA ZA VIONGOZI

**61.** Tume ya Tabia ya Viongozi ya Jamhuri ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 itakuwa na mamlaka ya kutekeleza shughuli zake Tanzania Visiwani kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 ya Sheria yoyote itakayotungwa chini ya Katiba hii na Bunge au na Baraza la Wawakilishi. Tume ya Tabia ya Viongozi.

## SURA YA NANE

### Masharti Kuhusu Mambo ya Fedha Zinazohusika na Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Masharti ya kutoza kodi.

**62.** Kodi ya aina yoyote isiyohusikana na mambo ya Jamhuri ya Muungano haitatozwa isipokuwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu ya kisheria na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa mamlaka na madaraka yake.

Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**63.**—(1) Fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zitawekwa katika mfuko mmoja maalum ambao utaitwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Fedha ambazo hazitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ni zile zote ambazo zimetajwa na Sheria kwamba zitumike kwa shughuli maalum au ziwekwe katika mfuko mwingine kwa ajili ya matumizi maalum.

Masharti ya kutoa fedha za matumizi kutoka Mfuko Mkuu.

**64.**—(1) Fedha hazitatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya matumizi ila kwa mujibu wa masharti yafuatayo—

(a) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na idhini hiyo iwe imetolewa chini ya Katiba hii au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahsusi na Baraza la Wawakilishi au Sheria iliyotungwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 67 ya Katiba hii.

(2) Fedha zilizomo katika mfuko maalum wowote wa Serikali, ukiachilia mbali Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, hazitatolewa kutoka mfuko huo kwa ajili ya matumizi ila mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na Sheria.

(3) Fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hazitatolewa kutoka Mfuko huo kwa ajili ya matumizi ila mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na pia kwa sharti kwamba fedha hizo ziwe zimetolewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

**65.**—(1) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atatoa maagizo kwa watu wanaohusika kwamba watengeneze na kuwasilisha kwenye Baraza la Wawakilishi katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya Baraza la Wawakilishi kuyakubali Makadirio ya Matumizi (mbali na matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Katiba hii au Sheria nyingine yoyote kuwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali) kutawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi Muswada, ambao utaitwa Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, na fedha hizo zitakazotolewa kulipia gharama za shughuli mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinazohusika na Makadirio hayo.

(3) Ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba—

(a) fedha za matumizi zilizoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya shughuli fulani hazitoshi au kwamba imekuwa lazima kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa Sheria; au

(b) kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli fulani kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi yaliyoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo au kwamba fedha zimetumiwa kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa Sheria, kutawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Matumizi na nyongeza au, kadiri itakavyokuwa, Maelezo ya Matumizi ya Ziada, na baada ya Baraza la Wawakilishi kuyakubali hayo Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza au Maelezo ya Matumizi ya Ziada, kutawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, na fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika na hayo Makadirio au Maelezo.

**Kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria kuanza.**

**66.**—(1) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kufuata utaratibu uliolezwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii.

(2) Iwapo mwaka wa fedha wa Serikali umeanza na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali inayohusika na mwaka huo haijaanza kutumika, basi Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kuidhinisha fedha itolewe kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya kulipia gharama za lazima za shughuli za Serikali, na fedha hizo zitatumiwa mpaka ipite miezi minne tangu mwanzo wa mwaka wa fedha au mpaka Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali itakapoanza kutumika, kutegemea ni lipi kati ya mambo hayo litakalotokea mapema zaidi.

Mfuko wa Matumizi ya Dharura.

**67.**—(1) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo—

(a) kuanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na kumwezesha Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar au Waziri aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili hiyo kuazima fedha kutoka mfuko huo kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura ambalo halikutazamiwa kutokea na ambalo halikupangiwa fedha zozote za matumizi; na

(b) kumwezesha Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar au Waziri aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwa ajili hiyo kutumia fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya shughuli fulani kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura kama ilivyoelezwa katika aya ya (a) ya ibara hii ndogo.

(2) Iwapo fedha zimeazimwa kutoka Mfuko wa Matumizi ya Dharura au fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya shughuli fulani zimetumiwa kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura, basi kutawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza, na baada ya Baraza la Wawakilishi kuyakubali Makadirio hayo Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali utakaowasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuidhinisha Matumizi hayo ya nyongeza utahakikishwa kwamba fedha zozote zilizoazimwa kutoka Mfuko wa Matumizi ya Dharura zitarudishwa kwenye Mfuko huo kutokana na fedha za matumizi yatakayoidhinishwa na Muswada huo.

Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**68.**—(1) Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa ibara hii, deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maana yake ni deni lenyewe na pia faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni pole pole na gharama zile zinazoambatana na usimamizi wa deni hilo.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**69.**—(1) Kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na jukumu juu ya mambo yafuatayo—

(a) kuhakikisha kwamba fedha zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 64 ya Katiba hii, na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

(b) kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika, zimetumiwa kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

(c) angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hesabu za Idara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahakama zote za Zanzibar na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na kila mtumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, kumbukmbu, hati za maelezo, taarifa na hati nyenginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yoyote iliyotajwa katika ibara ndogo ya pili (2) ya ibara hii.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kila taarifa atakayotowa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya (2) ya ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitakachofanyika baada ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kupokeya taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar hatachukuwa hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Kaimu Spika ambae atawasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi.

(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa pia na jukumu la kutekeleza kazi na shughuli nyingine, na atakuwa na madaraka mengine ya namna mbali mbali, kama itakavyoelezwa na sheria, kuhusu hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au hesabu za Mashirika na Makampuni ya Umma ya Zanzibar.

(6) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2), (3) na (4) ya ibara hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwengine yeyote au ibara yoyote ya Serikali, lakini maelezo hayo

ya ibara hii ndogo hayataizuia Mahakama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au au sivyo.

Kumuondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

**70.**—(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara hii. Vinginevyo ataendelea na kazi hiyo hadi kutimiza umri wa kuacha kazi kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Iwapo suala la kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa masharti ya ibara hii lahitaji kuchunguzwa, basi utaratibu ufuatao ndio utakaotumika—

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atateua Tume Maalum ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili wote wenye sifa zinazofaa kama viongozi katika Chama na Serikali wenye uzoefu wa kutosha katika fani mbali mbali za shughuli hizo;

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kuhusu maelezo ya shauri lote pamoja na ushauri wao kama huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(3) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) itamshauri Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar atamwondoa kazini.

(4) Na kwa hali yoyote Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar anaweza kutumia busara yake ikiwa Tume itamshauri kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu asiondolewe kazini.

(5) Mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu au aliyepata kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## SURA YA TISA

### MADARAKA MIKOANI—KAMATI YA MAPINDUZI

**71.** Kutakuwa na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila Mikoa, Wilaya au Eneo ambavyo vitajulikana kama Kamati za Mapinduzi ambazo shughuli na madaraka yake yameelezwa katika sheria ya Kamati za Mapinduzi ya 1979. Serikali za Mitaa. Sheria Nam. 1 ya 1979

**72.** Kamati za Mapinduzi kama ni Serikali za Mikoa, Wilaya na Maeneo zitahusika kwa ujumla na shughuli zifuatazo:— Kazi za Kamati za Mapinduzi.

(a) Kutekeleza kazi za Serikali za mitaa katika maeneo, Wilaya na Mikoa inayohusika;

(b) Kuhakikisha uimarishaji wa amani, utekelezaji wa sheria na ulinzi wa Wananchi.

(c) Kusaidia kwa kadri iwezekanavyo katika utekelezaji na usimamiaji wa mipango ya maendeleo au miongozo yoyote ya Serikali katika Mkoa, Wilaya au eneo.

(d) Kuendeleza siasa ya Ujamaa pamoja na kuendeleza Mapinduzi katika Mikoa, Wilaya na Maeneo.

(e) Kuwashirikisha kikamilifu Wananchi wote katika Mikoa, Wilaya na Maeneo yanayohusika katika mipango ya maendeleo ya uchumi kama zenyewe inavyobuniwa na Serikali au Kamati zenyewe kwa madhumuni ya kunyanyua hali ya maisha ya wananchi;

(f) kuyaelewa mahitaji muhimu ya wananchi pamoja na mahitaji mengineyo, katika Mikoa, Wilaya au maeneo yao na kuhakikisha kwamba mahitaji hayo yanapatikana kutoka katika sehemu inayohusika Serikalini au kutokana na mipango ya kujitegemea wenyewe;

(g) Kutoa mapendekezo kuhusu utekelezaji wa miongozo ya Serikali au Mipango ya maendeleo katika Mikoa, Wilaya au Maeneo yanayohusika kwa kupitia katika Wizara, Idara au Mashirika yanayohusika au kwa kuwatumia watumishi wa Umma waliomo katika kamati;

(h) Katika utekelezaji wake wa kazi, Kamati ya Mapinduzi au Kamati Ndogo inaweza, inapoona kua ni lazima, kumwita mtumishi wa Umma yeyote kuhudhuria mkutano wa kamati kwa madhumuni ya kupata maoni, msaada au ufafanuzi toka kwa mtumishi huyo kuhusiana na jambo lolote lihusikalo na kazi zake katika Mkoa, Wilaya au Eneo lolote, hiyo itafanyika kwa kutumia utaratibu unaostahiki kupitia Wizara, Idara au Mashirika ya Umma yanayohusika.

## SURA YA KUMI

### TUME YA UCHAGUZI SERIKALI YA ZANZIBAR

Tume ya Uchaguzi.

**73.**—(1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao—

(a) Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atakuwa Mwenyekiti; na

(b) wajumbe wengine wasiopungua watatu na wasiozidi watano ambao watateuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar.

(2) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kumteua Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi toka miongoni mwa wajumbe aliowateua kwa mujibu wa masharti ya aya ya (b) ya ibara ndogo ya (1) ya ibara hii.

(3) Makamu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ataendelea kuwa Makamu wa Mwenyekiti kwa muda wote ataokuwa Mjumbe wa Tume, lakini Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza kufuta uteuzi wa Makamu wa Mwenyekiti na kumteua Mjumbe mwingine wa Tume kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi.

(4) Watu wafuatao hawataweza kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi, yaani—

(a) Memba wa Baraza la Mapinduzi;

(b) Naib Waziri;

(c) mtu mwenye madaraka ya aina yoyote iliyotajwa mahsusi na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwamba ni mwiko kwa mtu mwenye madaraka hayo kuwa Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi;

(d) Mjumbe Mwakilishi.

(5) Bila ya kuathiri masharti mengine yaliyomo katika ibara hii, Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi ataacha kuwa Mjumbe litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo—

(a) ukimalizika muda wa miaka mitano tangu alipoteuliwa; au

(b) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe wa Tume, lingemfanya asiweze kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi.

(6) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar aweza tu kumwondoa katika madaraka mjumbe wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya.

(7) Tume ya Uchaguzi yaweza kutekeleza shughuli zake bila ya kujali kwamba kuna nafasi iliyo wazi miongoni mwa viti vya wajumbe au kwamba mjumbe mmojawapo hayupo, lakini kila uamuzi wa Tume ni lazima uungwe mkono na wajumbe walio wengi kati ya wajumbe wote wa Tume.

(8) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kuwateua wajumbe wa kusimamia uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na, bila ya kuathiri masharti ya Sheria kama hiyo au maagizo ya Tume ya Uchaguzi, madaraka ya Tume ya Uchaguzi ya kusimamia uchaguzi yaweza kutekelezwa na wajumbe hao.

(9) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au ya Idara yoyote ya Serikali.

(10) Hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### IDARA MAALUM KWA SHUGHULI ZA ZANZIBAR
### JESHI LA KUJENGA UCHUMI, KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO NA CHUO CHA MAFUNZO

Idara Maalum za Serikali ya Zanzibar.

**74.**—(1) Kutakuwa na Idara maalum kwa ajili ya shughuli za Zanzibar ambazo zimeundwa kwa mujibu wa masharti ya sheria zinazohusika.

(2) Idara maalum zinazohusika chini ya ibara ndogo ya (1) ya kifungu hiki ni—

Jeshi la Kujenga Uchumi. Sheria Nam. 1 ya 1979

(a) Jeshi la Kujenga Uchumi (J.K.U) kama lilivyoundwa na Sheria ya Jeshi la Kujenga Uchumi, 1979.

Kikosi Maalum Sheria Nam. 13 ya 1979

(b) Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kama kilivyoundwa na Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, 1979;

Chuo cha Mafunzo. Sheria Nam. 2 ya 1972

(c) Chuo cha Mafunzo kama kilivyoundwa na Sheria ya Chuo cha Mafunzo 1972.

## SURA YA KUMI NA MBILI

### UFAFANUZI

Utaratibu wa kujiuzulu kwa mwenye madaraka yoyote chini ya Katiba hii.

**75.**—(1) Kwa madaraka na kazi yoyote iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba hii, mtu yeyote mwenye dhamana ya kazi hiyo aweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa iliyoandikwa na kutiwa sahihi kwa mkono wake kwa utaratibu ufuatao—

(a) atawasilisha taarifa hiyo ya kujiuzulu kwa mtu au mamlaka iliyomteua;

(b) ikiwa anayehusika na kujiuzulu ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, taarifa ya kujiuzulu ataiwasilisha kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama;

(c) ikiwa mtu huyo ni Memba wa Baraza la Mapinduzi au Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar taarifa ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar;

(d) ikiwa mtu huyo ni Spika taarifa ya kujiuzulu ataiwakilisha kwenye Baraza la Wawakilishi; na

(e) ikiwa mtu huyo ni Mjumbe Mwakilishi taarifa ya kujiuzulu ataiwakilisha kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Taarifa ya kujiuzulu itahesabika kikamilifu tangu siku ambayo taarifa hiyo imepokelewa na mtu au mamlaka inayohusika au ikiwa imetaja kuwa kujiuzulu huko ni tangu siku nyingine baada ya kupokelewa kwa taarifa hiyo kujiuzulu kutahesabika tangu siku hiyo nyingine iliyotajwa.

(3) Ikiwa mtu huyo anayehusika na kujiuzulu katika madaraka yoyote yanayohusika kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1) ya ibara hii bado anazo sifa zinazohitajika kwa kazi hiyo. kujiuzulu huko hakutakuwa kizuizi cha kuteuliwa au kuchaguliwa tena kushika madaraka ya aina hiyo.

Utaratibu wa kuteua mtu kushika madaraka kwa muda.

**76.** Mbali na madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar; Waziri au Naibu Waziri au Memba wa Baraza la Mapinduzi, mtu yeyote au mamlaka inayohusika kwa mujibu wa Katiba hii na uteuzi au uchaguzi wa mtu mwingine kushika madaraka ya kazi fulani anao pia uwezo wa kumteua au kumchagua Kaimu au mtu ambaye atashikilia kwa muda na kutekeleza madaraka ya kazi hiyo.

Utaratibu wa Sheria za Muungano kutumika Zanzibar.

**77.** Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitatumika Zanzibar ila kwa mujibu wa masharti ya aya (h) ya ibara ndogo (2) ya ibara ya 94 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977.

Tume ya Uchaguzi.

**78.** Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano itafanya kazi zake Zanzibar kwa mujibu wa maelezo ya kifungu cha 91 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977 kwa uchaguzi unaohusika na shughuli zake Tanzania Visiwani.

**79.**—(1) Suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba hii iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa litatanzuliwa na Kikao Maalum cha Mahakama Kuu ya Zanzibar.

(2) Kikao Maalum cha Mahakama Kuu ya Zanzibar maana yake ni kikao cha Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar wasiopunguwa watatu.

(3) Kila uamuzi utakaotolewa na Kikao Maalumu cha Mhakama Kuu ya Zanzibar kwa mujibu wa ibara hii utakuwa ndio wa mwisho, hakutakuwa na haki ya kukata rufaani kupeleka popote.

Ufafanuzi

**80.** Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yahitaji vinginevyo—

"Chama" maana yake ni Chama cha Mapinduzi (C.C.M. kwa kifupi).

"Mahkama Kuu" maana yake ni Mahakama Kuu ya Zanzibar.

"Mbunge" maana yake ni Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

"Mjumbe Mwakilishi" au "Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi" maana yake ni Mjumbe aliyechaguliwa au kuteuliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambalo shughuli zake ni za Bunge kwa shughuli za Zanzibar.

"Waziri" maana yake ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Memba wa Baraza la Mapinduzi aliyekabidhiwa wadhifa wa kazi ya Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Zanzibar" maana yake ni sawa na Tanzania Visiwani ikiwa ni Sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zamani ikijulikana kama Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Jina kamili la Katiba na tarehe ya kuanza kutumika Katiba.

**81.**—(1) Jina kamili la Katiba hii ni Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Katiba hii itaanza kutumika tarehe itakayotangazwa katika Gazeti la Serikali.